# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 15 | Desemba 11, 2022 JARIDA LA JUMAPILI BILA MALIPO





# De La Rue yakabili KRA

**Kampuni ya Uingereza ya kuchapisha pesa inatumia njia za kidiplomasia kumshawishi Rais William Ruto kuingilia kati mzozo wa Sh3.8 bilioni kati yake na shirika la ushuru huku ikitafuta kandarasi zaidi za biashara Kenya**

# The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore

# anywhere, anytime.


Follow the link to subscribe

> *epaper.nation.africa.*

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play




Nation

Nation

Nation Africa

For customer support Tel: 0790 111 111
Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**7 MAANDAMANO YANARUDI?** Ingawa kiongozi wa Azimio Raila Odinga ametaja mikutano yake kuwa mashauriano ya umma, wengi wanaamini ni mwanzo wa mvutano wa kisiasa wa muda mrefu.

**8 ABAUTANI YA ATWOLI:** Akihofia viongozi wakuu wa jamii ya Waluhya Moses Wetang'ula, Musalia Mudavadi na wengine watamtenga na siasa za eneo la Magharibi, kiongozi wa vyama vya wafanyakazi anyenyekea na kubadilisha wimbo kutoka "Ruto hatawahi kuwa Rais" hadi kummiminia sifa kiongozi wa Kenya Kwanza.

**11 ANAFUATA UPEPO?** Aliyekuwa rais wa Afrika Kusini Jacob Zuma aendelea na mashtaka ya kibinafsi dhidi ya mwendesha mashtaka mkuu wa serikali na mwanahabari katika kile wachanganuzi wanataja kuwa juhudi zisizoweza kufaulu.




**15 MUSK AZONGWA NA KESI:** Kufuta kazi wafanyakazi 7,500 wa Twitter kunaweza kumgeukia Elon Musk, anayekabiliwa na kesi nyingi kuhusu masharti ya kuwaachisha kazi watu wengi baada ya kununua mtandao huo mkubwa wa kijamii.

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

# Kazi za IEBC zisitumiwe kuangamiza taaluma za watu, tunahitaji siasa safi

Kufanya kazi katika IEBC hakutaki watu walio na moyo dhaifu. Unapokubali kazi kama kamishna wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), unaanza kujiandaa kuondoka.

Katika muda wa miaka sita pekee, makamishna 16 wametimuliwa kabla ya mihula yao kukamilika.

Kila uchaguzi unafuatiwa na miito ya kutaka makamishna wa tume hiyo wajiuzulu, hasa miito hiyo hutoka upande unaoshindwa.

Wote huwa wanatimuliwa kwa kulimbikiziwa wingu la madai, kuharibu kazi na taaluma zao wanazojenga kwa miongo mingi. IEBC, bila shaka, ni shirika la kisiasa tu. Ni tume inayosimamia mashindano ya kisiasa, na kuamua watakaoshikilia nyadhifa kubwa za kisiasa nchini.

Katika nchi kama Kenya ambapo wanasiasa wanachukuliwa kama miungu, si ajabu kwamba huwa kuna mvutano mkubwa wakati wa kuajiri makamishna wa IEBC.

Kila mwanasiasa hushuku mwegemeo wa kisiasa wa makamishna, na kufanya kazi yao kuwa ngumu sana.

Mzozo wa hivi punde katika tume hiyo kufuatia uchaguzi mkuu wa Agosti 9 ni mkubwa, hata kushinda uliotokea 2018 makamishna wanne walipojiuzulu kwa wakati mmoja.

Makamishna watatu, akiwemo mwenyekiti wao, walionekana kuegemea mrengo mmoja wa kisiasa huku wengine wanne wakionekana kupendelea mrengo mwingine.

Migawanyiko hiyo ilionekana hadharani, kwa mshangao wa



**Washington Gikunju**

Katika nchi kama Kenya ambapo wanasiasa wanachukuliwa kama miungu, si ajabu kwamba huwa kuna mvutano mkubwa wakati wa kuajiri makamishna wa IEBC. Kila mwanasiasa hushuku mwegemeo wa kisiasa wa makamishna, na kufanya kazi yao kuwa ngumu sana. Wanasiasa waonyeshe nia nzuri na kukubali hali ya kupata wanayotaka na hata kukosa baadhi, ili kukubaliana kuhusu uajiri wa makamishna..

nchi iliyofuatilia kesi ya uchaguzi wa urais katika Mahakama ya Upeo.

Na mwishowe, hata mahakama ya juu zaidi ilikataa kufafanua suala la athari za mgawanyiko miongoni mwa makamishna kuhusu matokeo ya uchaguzi.

Ilionekana kuwa hata waheshimiwa majaji, bila kutaja waziwazi, walichukulia suala hilo kuwa la kisiasa ambalo linaweza kutatuliwa tu kupitia mchakato wa kisiasa na sio wa mahakama.

Katika barua aliyoandikia Rais Ruto mnamo Alhamisi, Kamishna Francis Wanderi alimlaumu mwenyekiti Wafula Chebukati kwa kuwa na "mkaidi na mwenye tabia ya kidikteta", na akasema uongozi wake "haukuwa wa misingi ya usimamizi bora".

Madai hayo yanalingana na yaliyoibuliwa na makamishna wa zamani wa IEBC waliojiuzulu 2018, wakidai kuwa chini ya uongozi wa Chebukati "ukumbi wa mikutano wa tume umekuwa eneo la kueneza habari za uongo, mahali kwa kutoaminiana na eneo la kung'ang'ania na kutafuta sifa na umaarufu wa kibinafsi".

Na hapa ndipo shida ilipo. Kushukiana miongoni mwa makamishna kumekita mizizi, hasa kwa sababu kila mmoja anaonekana kuwakilisha mirengo tofauti ya kisiasa. Serikali ya Rais Ruto inapaswa kujifunza kutokana na historia, katika juhudi za sasa za kubadilisha sheria zinazohusu uajiri wa makamishna.

Mabadiliko yanayopendekezwa yanafaa kuhusisha kila upande, na kushirikisha majadiliano mapana katika Bunge na Mashirika ya Kijamii.

Mwisho, ni lazima wanasiasa waonyeshe nia nzuri na kukubali hali ya kupata wanayotaka na hata kukosa baadhi, ili kukubaliana kuhusu uajiri wa makamishna.

**wgikunju@ke.nationmedia.com**

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini ya Wiki
Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno
**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Mahojiano kuendelea wiki hii

## Havi awania wadhifa wa Wakili Mkuu

Aliyekuwa mwenyekiti wa Chama cha Mawakili Kenya (LSK) Nelson Andayi Havi atakuwa miongoni mwa watu wanane ambao watafika mbele ya Tume ya Utumishi ya Umma (PSC) kuhojiwa kwa wadhifa wa Wakili Mkuu wa Serikali.

Tume inataka kujaza nafasi ya Kennedy Ogeto, aliyeteuliwa wakati wa utawala wa Rais mstaafu Uhuru Kenyatta.

Mahojiano hayo yatakuwa Jumanne na Jumatano wiki hii na jina la atakayefaulu litawasilishwa kwa Rais William Ruto, ambaye ataliwasilisha kwa Bunge la Kitaifa kupigwa msasa na kuidhinishwa.

Wanaotarajiwa kufika mbele ya PSC ni aliyekuwa Mbunge wa Kitutu Masaba Shadrack Mose, Marykaren Kigen Sorobit, Beatrice Adhiambo Akuno, Paul Lilan, Beatrice Mugeni Meso, Stephen Ochieng Mallowah na George Kithi.

Orodha hiyo ilifichuliwa wiki mbili zilizopita na tume hiyo na umma ukapewa hadi Desemba 8, 2022 kuwasilisha maoni au malalamishi kuhusu walioorodheshwa. Muhula wa Ogeto unaisha Machi 2023.

■ Kenya, Benki ya Dunia zazindua mfumo wa ushirika



Mkurugenzi wa Benki ya Dunia wa Kenya, Rwanda, Somalia na Uganda Keith Hansen akiongea jijini Nairobi mnamo Desemba 6 wakati wa uzinduzi wa Mfumo wa Ushirika wa Nchi. PICHA | DENNIS ONSONGO

■ Mankuli ya mchana ya walimu Mombasa



Wajumbe wakifurahia nyamachoma siku ya pili ya Kongamano la 18 la Chama cha Walimu wa Shule za Msingi Kenya katika ukumbi wa Sheikh Zayed, mjini Mombasa mnamo Desemba 6. PICHA | KEVIN ODIT

## Tume yatangaza nafasi 35,550 za walimu

TUME ya Kuajiri Walimu (TSC) wiki hii itaanza kuajiri zaidi ya walimu 30,000 kwa ajili ya kuanzishwa kwa shule za upili za kimsingi kuanzia Januari mwaka ujao.

TSC imetangaza nafasi 9,000 za walimu katika shule za upili za umma na nafasi 1,000 katika shule za msingi za umma. Walimu hawa 10,000 wanaajiriwa kwa mpango wa kudumu na kulipwa pensheni.

Wengi wa walimu hao wapya, wataajiriwa kama vibarua. Walimu hawa 21,550, watafunza katika shule za upili za kimsingi, ambazo kulingana na tangazo la na Rais William Ruto wiki iliyopita, zitakuwa katika shule za msingi.

Walimu wengine 4,000 vibarua wataajiriwa kufunza katika shule za msingi za umma.

Kuweka wanafunzi wa shule za upili za kimsingi katika shule za msingi ni uamuzi wa kisera unaokinzana na uamuzi wa serikali iliyopita ya Jubilee kuwa wanafunzi wa Gredi 7, Gredi 8 na Gredi 9 wasomee katika shule za upili.

Mpango wa kuajiri walimu 30,000 unafungamana na ahadi ya muungano wa Kenya Kwanza nyakati za kampeni iliyolenga kupunguza kero la uhaba wa walimu katika shule za umma nchini.

Walimu wa shule za upili wanahitajika kuwa na angalau uhitimu wa shahada ya diploma katika taaluma ya ualimu na umilisi wa ufundishaji wa masomo manne ya kutahiniwa.

■ Bei zilipanda asilimia 0.3 mwezi uliopita

## Hisa Amerika zapungua, bei yapanda



Hisa katika soko la fedha la Wall Street, Ijumaa zilishuka baada ya bei ya jumla Amerika kupanda zaidi ya ilivyotarajiwa, na kuongeza hofu kuhusu iwapo mfumuko utaendelea kupungua. Punde baada ya uuzaji kuanza, hisa za Dow Jones Industrial Average zilishuka kwa asilimia 0.2 hadi 33,713.50. Nazo hisa za S&P 500 zilishuka kwa asilimia 0.3 hadi 3,953.36, huku za Nasdaq Composite Index zikupungua kwa asilimia 10.3 hadi 11,045.39. Hasara hiyo ilijiri baada ya Idara ya Leba kuripoti kuwa bei za uzalishaji ziliongezeka kwa asilimia 0.3 Novemba zaidi kidogo ya ilivyotarajiwa.

■ Umoja wa Uarabu wasikika Doha, Qatar

## Ushindi wa Morocco walegeza uhasama



Jezi inayouzwa kwenye lango la soko kuu jijini Doha inatangaza "Damu yetu ni Kiarabu", na hali hii ya hisia inatia moyo Morocco ambayo imekuwa nchi ya kwanza ya Kiarabu kucheza katika robo fainali za Kombe la Dunia. Uhasama wa kikanda ulisahaulika. Bendera ya Morocco rangi nyekundu na nyota ya kijani kibichi iliuzwa kwa wingi kote Doha kabla ya mechi yake na Ureno.

Bendera hiyo, pamoja na zile za Qatar, Tunisia na Saudi Arabia – ziko katika jezi zenye maandishi "Damu yetu ni Kiarabu" zinazouzwa katika soko la Souq Waqif, jijini Doha. Qatar imekuwa ikionyesha michezo hiyo kama ya kujivunia Uarabu.

*- Zimetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

■ MABILIONI YA PESA ZA STAMPU ZA SERIKALI YAPIGANIWA

# SAKATA YA DE LA RUE

## Kampuni ya Uingereza yatumia uhusiano wa kidiplomasia kutatua mzozo wa ushuru na kushinda kandarasi nchini Kenya



Serikali ya Waziri Mkuu mpya wa Uingereza Rishi Sunak majuzi ilituma ujumbe wa maafisa wakuu nchini Kenya wakiongozwa na Waziri wa Mashauri ya Kigeni, James Cleverly.

● Na JAINDI KISERO

Kwa wakati huu, diplomasia ya kisasa inakumbwa na mageuzi makubwa. Badala ya kujitosa kwenye ushindani wa kimataifa kushinda kandarasi barani Afrika, inaonekana kwamba kampuni kubwa za bara Ulaya sasa zinaamua kuweka presha ya kidiplomasia kwa serikali ili kupata kandarasi.

Imeibuka kwamba kampuni ya kuchapisha noti za pesa ya Uingereza, De La Rue PLC, sasa inaweka presha za kidiplomasia kwa serikali mpya ya Rais William Ruto iingilie kati kuipendelea katika mzozo wa muda mrefu kati yake na Mamlaka ya Ushuru ya Kenya (KRA) kuhusu ushuru wa thamani ya Sh 3.8 bilioni.

Mbinu za kampuni hiyo ya kimataifa ya kuchapisha pesa imeibua tetesi kwa kuwa ni nadra sana kuona kampuni kubwa ya kimataifa ikiamua kutumia shinikizo za hali ya juu za kidiplomasia kutatua mizozo ya ushuru hasa kuhusu masuala ambayo hayamo katika mikataba ya ushuru na katika hali ambayo baadhi ya masuala yanahusu kesi zilizo kortini.

Ni wazi kuwa De La Rue inatumia kinachoonekana kuwa enzi mpya za kuimarika kwa uhusiano kati ya Uingereza na Kenya kufuatia mazungumzo ya hali ya kidiplomasia kati ya Rais William Ruto na Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak ambapo viongozi hao wawili waliahidi kuharakisha uwekezaji wa Uingereza nchini Kenya. Hii ilifuatiwa na ziara ya wiki hii Nairobi ya Waziri wa Mashauri ya Kigeni, James Cleverly. Kulingana na mawasiliano yaliyoonekana na Darubini ya Wiki, maafisa wakuu wa kampuni hiyo walitembelea Ubalozi wa Kenya jijini London kuwasilisha malalamishi kuhusu KRA.

Kutokana na malalamishi hayo, Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda imeingilia kati kwa kushinikiza KRA kutoa maelezo kuhusu malalamishi ya kampuni hiyo ya uchapishaji.

Mawasiliano yanaonyesha kuwa Afisa Mkuu Mtendaji wa De La Rue, Bw Clive Vacher, alitarajiwa Nairobi wiki hii kukutana na maafisa wakuu wa serikali mpya kujadili masuala ya ushuru kati ya kampuni na mamlaka hiyo ya ushuru nchini.

Hali kwamba ziara hiyo ilipangwa wakati mmoja na ziara ya Bw Cleverley Nairobi haiwezi kuwa sadfa. Mojawapo wa masuala yanayoshughulikiwa ni kesi ya miaka mingi kuhusu Ushuru wa Ziada wa Mapato (VAT) ambao De La Rue inasisitiza haikufaa kutozwa na ambao mnamo Mei 2021, Baraza la Mahakama kuhusu Ushuru liliamua kwamba De La Rue ilipaswa kulipa.

Kesi hiyo ya ushuru wa thamani ya Sh 1.2 bilioni ilipangwa kusikizwa katika Mahakama Kuu Desemba 8.

Kesi ya pili - ya miaka mingi na shirika hilo, kuhusu ushuru wa kutoka 2013 hadi 2017, uliokuwa wa thamani ya Sh 1.1 bilioni, ilisikizwa katika Mahakama Kuu mnamo Machi 2022 na uamuzi unatarajiwa kutolewa wakati wowote kuanzia sasa. KRA ilishinda kesi hiyo mbele ya Baraza la

Endelea Uk 6

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

# Uingereza yatumia diplomasia kupata biashara

Kutoka Uk 5

Mahakama Kuhusu Ushuru mnamo Mei 2021.

Kesi ya tatu inayohusu ushuru wa mapato wa thamani ya Sh1.5 bilioni ambayo kwa wakati huu inashughulikiwa kwa njia mbadala za kutatua kesi- inayohusu juhudi za kutatua mizozo kabla ya kesi kuwasilishwa kwa Baraza la Mahakama Kuhusu

Ushuru.

De La Rue imeonyesha nia ya kutatua kesi hiyo lakini pande zote hazijakubaliana kuhusu kiasi kinachopaswa kulipwa kama mirahaba.

Mawasiliano hayo ya barua pia yanaonyesha kuwa De La Rue inatumia nguvu za kibalozi kupata zabuni ya mabilioni ya pesa ya kuchapisha stampu za ushuru.

Darubini ya Wiki imeona mawasiliano ambapo De La Rue imefahamisha serikali kupitia kwa barua kwamba haijaweza kupata faida kutoka kwa kandarasi za kuchapisha noti za pesa ambazo imekuwa ikitengewa na Benki Kuu ya Kenya.

Kuna kiini cha kuzuka kwa mizozo hii. Mnamo 2019, Serikali iliweka mkataba na De La Rue ambapo serikali ililipa Sh700 milioni kupata asilimia 40 ya kampuni hiyo. Lakini kwa wakati huu De La Rue inaambia serikali kuwa, baada ya mkataba huo kukamilika, kiwanda chake nchini Kenya hakijawahi kupata faida au kulipa mgao kwa wenyehisa kwa madai kuwa haijawahi kupata nafasi ya mradi mkubwa wa kuchapisha stampu za usalama za mashirika ya serikali, ikiwemo KRA, Shirika la Ukadiriaji wa Bidhaa Kenya (Kebs) na Kadi za Huduma.

Kulingana na jinsi serikali ya Rais Ruto itashughulikia shinikizo kutoka nchi iliyotawala Kenya wakati wa ukoloni kuhusu suala la kandarasi za stampu za ushuru, jukwaa tayari limewekwa kwa ushindani mkali na kampuni ya Uswizi, SICPA, ambayo imekuwa ikipata kandarasi hiyo kwa miaka mingi.


Hivi majuzi, Rais Ruto alilalamika vikali kuhusu idadi ya stampu za ushuru zinazouzwa Kenya, na kuibua shaka kwamba usaidizi wa kisiasa ambao kampuni hiyo ya Uswizi imekuwa ikifurahia chini ya utawala wa Rais Kenyatta umeanza kufifia.

Mwaka uliopita, KRA iliongeza kimya kimya mkataba uliopo wa miaka 7 na Sicpa kupatia kampuni hiyo ya Uswizi kandarasi zote za kuchapisha stampu.

Lakini pengine kinachoelezea vyema kiwango cha juu cha usaidizi wa kisiasa ambacho kampuni hiyo ya Uswizi imekuwa ikifurahia chini ya serikali ya Rais Kenyatta ni njama ya kamati iliyoshirikishwa kutoka Afisi ya Rais kwa jina refu la Kundi la Kiufundi la Mashirika tofauti Kuhusu Mfumo Uliopendekezwa wa Kuweka Alama Bidhaa na Kuzithibitisha. Kamati hii ilipendekeza kuanzisha kitu kinachoitwa "Alama Jumuishi ya Serikali ya Kenya".

Kwamba, badala ya hali ya sasa ambapo mashirika kadhaa, ikiwemo KRA, Kebs, KEPHIS, na Mamlaka ya Kupambana na Bidhaa Feki yanayohusika na uthibitishaji wa bidhaa na utoaji wa stampu za ushuru, Kenya ilichohitaji ni mfumo mpya ambapo uidhinishaji wa bidhaa na stampu za ushuru zinapaswa kuwekwa pamoja na kuendeshwa katika jukwaa moja chini ya mfumo wa EGMS wa KRA unaosimamiwa na Sicpa.

Ili kufanikisha pendekezo hilo, kamati ilikuwa imetayarisha Mswada wa Alama Jumuishi ya Serikali ya Kenya, 2022, ambao ilikuwa utolewe na KRA. Bunge ilivunjwa kabla ya kujadili Mswada huo.



Rais William Ruto siku za hivi majuzi amekuwa akilalamika kuhusu idadi ya stampu za ushuru zinazouzwa na Mamlaka ya Ushuru Kenya. Jinsi atakavyoshughulikia juhudi za kidiplomasia katika suala la ushuru kuhusu De La Rue itatoa mwelekeo kuhusu biashara ya kampuni hiyo ya Uingereza nchini Kenya katika siku za usoni. PICHA | MAKTABA



James Cleverly, Waziri wa Mashauri ya Kigeni wa Uingereza, Jumuiya na Maendeleo akihojiwa Desemba 8.

Iwapo hii ilikuwa njama ya kupatia Sicpa ukiritimba wa kuchapisha stampu za mashirika yote ya serikali Kenya ni swali lililo na jibu wazi, mpango huo ulikuwa wa kunufaisha Sicpa pakubwa.

Kilinachofanya wadadisi kuamini kuwa mpango wa kuunda alama moja ya serikali ulikuwa dhihirisho lingine la usaidizi wa kisiasa ambao Sicpa ilifurahia chini ya utawala wa Rais Kenyatta ni ukweli kuwa, hata kabla ya sheria ya kuunda alama ya pamoja ya serikali ya Kenya kupitishwa, maamuzi yalikuwa yakifanywa haraka kuweka mashirika mengine chini ya mfumo wa EGMS uliosimamiwa na Sicpa.

Katika mpango huo mpya, KRA na Sicpa zimeahidi 'kuhakikisha mfumo wa EGMS unapatikana kutumiwa na mashirika mengine ya serikali'.

Na katika stakabadhi za kandarasi, kuna vipengee vinavyoeleza jinsi ya kutathmini bei ya mashirika mengine ya serikali ambayo yatakuwa yamejiunga na jukwaa la EGMS katika KRA.

Pia, kipengee kingine kinasema KRA na Sicpa zitatoa huduma za kusaidia uchunguzi na mashtaka kwa maafisa wa Kenya na mashirika ya utekelezaji.

Kwamba Sicpa na KRA zilitia saini mpango ambapo mfumo wa EGMS unaosimamiwa na Sicpa ungekuwa wa pekee kutoa stampu, zikiwemo bei - kwa mashirika mengine ni moja ya sehemu za kuvutia kuhusu sakata hii.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

KINARA WA ODM ASEMA RUTO ANATAKA IEBC ANAYOWEZA KUTUMIA

# MAANDAMANO YANARUDI?

## Mikutano ya hadhara ya Raila inalenga kuangazia mambo ambayo serikali imeshindwa kutimiza na kuyaweka katika mawazo ya umma



Kiongozi wa muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya Raila Odinga akihutubia mkutano wa hadhara katika uwanja wa kihistoria wa Kamukunji, jijini Nairobi mnamo Jumatano. PICHA | DENNIS ONSONGO

• Na KWENDO OPANGA

Mkuu wa Wafanyakazi, Francis Atwoli na Hazina ya Hasla ni mambo ambayo yameibua joto na kuzungumziwa zaidi ndani ya wiki mbili zilizopita.

Kwanza, ni kwa sababu alibadilika ghafla kutoka kuwa mkosoaji mkubwa wa William Ruto mgombeaji na kuwa mfuasi wa Ruto rais, na nyingine ni sababu watakaofaidi wanatarajia mikopo ambayo ni mara 10 ya kiwango walichopewa au wanachotarajia kuchukua.

Kwa mtazamo wangu, Ruto alipotangazwa Rais mteule mnamo Agosti 15, Atwoli alivalia kofia ya kutafakari na kuzamia hali mpya ya kisiasa nchini na miongoni mwa Waluhya na kile hali hiyo itamaanisha kwake kama Muluhya na kama kiongozi wa wafanyakazi katika ngazi za kitaifa, kikanda, ngazi ya bara na ulimwengu.

Katika ngazi hizi zote, Atwoli anajua, wema huanzia nyumbani.

Uamuzi wake ulikuwa wazi, maslahi yake na yale ya wafanyakazi yatalindwa vizuri akiingia ndani ya hema ya Ruto.

Alivyosema, upende usipende, Ruto atakuwa Rais ndani ya miaka mitano ijayo na inaweza kuwa vigumu kumuondoa 2027.

Atwoli atafurahi kuanzisha safari ya kuondoka katika uongozi wa wafanyakazi wa Kenya vyema, badala ya Ikulu kupanga kuondolewa kwake kwa njia isiyo ya heshima.

Pili, Atwoli anajua kuwa maslahi ya wafanyakazi katika Hazina ya Kitaifa ya Malipo ya Uzeeni na Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Hospitali, kwa mfano, na makubaliano yao kuhusu nyongeza ya mishahara, yatatetewa vizuri ndani au karibu na serikali badala ya kutoka mbali.

Atwoli amehudumu kataka tawala za marais Moi, Kibaki na Uhuru, rekodi ambayo inaweza kutamaniwa na mchezaji yeyote wa kisiasa.

Tatu, ikiwa Atwoli atasalia nje akiangalia ndani, basi Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetang'ula na Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi, anaowachukulia kuwa wanawe kisiasa, watalazimika kumsukuma nje ya serikali, ambako anaamini anafaa kuwa.

Kwa mtazamo mwingine, Atwoli yuko hapa na anaendeshwa zaidi na siasa za kivitendo badala ya zile zinazojikita katika masuala.

Kwa hivyo, kwa ujasiri amesalimu amri hadharani na kumkumbatia mtu ambaye alidai angejinyonga kwa sababu angeshindwa katika uchaguzi wa urais.

Na Rais ni muungwana katika ushindi kutambua kuwa kiongozi huyo mkongwe wa vyama vya wafanyakazi alikuwa na haki ya kumpigia debe mgombeaji urais aliyempendelea.

Lakini ni lazima Ruto ajitahidi kuhakikisha kuwa mradi wake wa Hazina ya Hasla, unafaulu. Ukifeli, Rais atalazimika kutoa jasho na kupambana vikali ili aweze kuchaguliwa tena.

Rais na mradi wake huo, ambao aliupigia debe wakati wa kampeni, amelaumiwa kwa kuwapa Wakenya "mkopo wa Sh500 kunyolewa badala ya kufungua biashara ya kinyozi."

Na Ruto amelaumiwa kwa kuahidi mkopo bila riba na ruzuku wakati wa kampeni, lakini akawasaliti mahasla ambao walikuwa wafuasi wake wakuu, baada ya kuingia mamlakani.

Viongozi wa upinzani, wakiongozwa na Raila Odinga, ambaye hazeeki, mwenye kukosea kila mara, Kalonzo Musyoka na mgumu kama kucha Martha Karua, wamekasirika na kupata njia ya kulemaza utawala huu mchanga.

Tawala, hasa zile changa, hupata shinda miradi yake mikuu inapokumbwa na shida na Ruto atafanya kila awezalo kuhakikisha vijana wanaopata Sh500, Sh700, na Sh1,000 wameanzisha biashara na wanalipa riba, wanakopa zaidi na kuimarika. La sivyo, itakuwa vigumu kunyamazisha sauti zinazosherehekea kuanguka kwa mradi huo.

Odinga, Musyoka na Karua wanasugua mikono yao kwa furaha kwa matarajio huku serikali ikijikaza kuelezea kiasi cha pesa kinachokopwa, hitaji la kulipa riba kila baada ya majuma mawili na kuvunjika moyo, hasa miongoni mwa vijana.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni




Nation Media Group "ePaper Copy"

KIONGOZI WA WAFANYAKAZI ANYEYEKEA

# Atwoli apiga abautani kulinda maslahi



KWENDO **OPANGA**

Mkuu wa Wafanyakazi, Francis Atwoli na Hazina ya Hasla ni mambo ambayo yameibua joto na kuzungumziwa zaidi ndani ya wiki mbili zilizopita.

Kwanza, ni kwa sababu alibadilika ghafla kutoka kuwa mkosoaji mkubwa wa William Ruto mgombeaji na kuwa mfuasi wa Ruto rais, na nyingine ni sababu watakaofaidi wanatarajia mikopo ambayo ni mara 10 ya kiwango walichopewa au wanachotarajia kuchukua.

Kwa mtazamo wangu, Ruto alipotangazwa Rais mteule mnamo Agosti 15, Atwoli alivalia kofia ya kutafakari na kuzamia hali mpya ya kisiasa nchini na miongoni mwa Waluhya na kile hali hiyo itamaanisha kwake kama Muluhya na kama kiongozi wa wafanyakazi katika ngazi za kitaifa, kikanda, ngazi ya bara na ulimwengu.

Katika ngazi hizi zote, Atwoli anajua, wema huanzia nyumbani. Uamuzi wake ulikuwa wazi, maslahi yake na yale ya wafanyakazi yatalindwa vizuri akiingia ndani ya hema ya Ruto.

Alivyosema, upende usipende, Ruto atakuwa Rais ndani ya miaka mitano ijayo na inaweza kuwa vigumu kumuondoa 2027.

Atwoli atafurahi kuanzisha safari ya kuondoka katika uongozi wa wafanyakazi wa Kenya vyema, badala ya Ikulu kupanga kuondolewa kwake kwa njia isiyo ya heshima.

Pili, Atwoli anajua kuwa maslahi ya wafanyakazi katika Hazina ya Kitaifa ya Malipo ya Uzeeni na Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Hospitali, kwa mfano, na makubaliano yao kuhusu nyongeza ya mishahara, yatatetewa vizuri ndani au karibu na serikali badala ya kutoka mbali.

Atwoli amehudumu kataka tawala za marais Moi, Kibaki na Uhuru, rekodi ambayo inaweza kutamaniwa na mchezaji yeyote wa kisiasa.

Tatu, ikiwa Atwoli atasalia nje akiangalia ndani, basi Spika wa Bunge la Kitaifa Moses Wetang'ula na Mkuu wa Mawaziri Musalia Mudavadi, anaowachukulia kuwa wanawe kisiasa, watalazimika kumsukuma nje ya serikali, ambako anaamini anafaa kuwa.

Kwa mtazamo mwingine, Atwoli yuko hapa na anaendeshwa zaidi na siasa za kivitendo badala ya zile zinazojikita katika masuala.

Kwa hivyo, kwa ujasiri amesalimu amri hadharani na kumkumbatia mtu ambaye alidai angejinyonga kwa sababu angeshindwa katika uchaguzi wa urais.

Na Rais ni muungwana katika ushindi kutambua kuwa kiongozi huyo mkongwe wa vyama vya wafanyakazi alikuwa na haki ya kumpigia debe mgombeaji urais aliyempendelea.

Lakini ni lazima Ruto ajitahidi kuhakikisha kuwa mradi wake wa Hazina ya Hasla, unafaulu. Ukifeli, Rais atalazimika kutoa jasho na kupambana vikali ili aweze kuchaguliwa tena.

Rais na mradi wake huo, ambao aliupigia debe wakati wa kampeni, amelaumiwa kwa kuwapa Wakenya "mkopo wa Sh500 kunyolewa badala ya kufungua biashara ya kinyozi."

Na Ruto amelaumiwa kwa kuahidi mkopo bila riba na ruzuku wakati wa kampeni, lakini akawasaliti mahasla ambao walikuwa wafuasi wake wakuu, baada ya kuingia mamlakani.

Viongozi wa upinzani, wakiongozwa na Raila Odinga, ambaye hazeeki, mwenye kukosea kila mara, Kalonzo Musyoka na mgumu kama kucha Martha Karua, wamekasirika na kupata njia ya kulemaza utawala huu mchanga.

Tawala, hasa zile changa, hupata shinda miradi yake mikuu inapokumbwa na shida na Ruto atafanya kila awezalo kuhakikisha vijana wanaopata Sh500, Sh700, na Sh1,000 wameanzisha biashara na wanalipa riba, wanakopa zaidi na kuimarika. La sivyo, itakuwa vigumu kunyamazisha sauti zinazoshereheshekea kuanguka kwa mradi huo.

Odinga, Musyoka na Karua wanasugua mikono yao kwa furaha kwa matarajio huku serikali ikijikaza kuelezea kiasi cha pesa kinachokopwa, hitaji la kulipa riba kila baada ya majuma mawili na kuvunjika moyo, hasa miongoni mwa vijana.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy"

maoni

Kenya Kwanza yahukumiwa na umma

# Marufuku ya shule za mabweni isiwaumize wazazi



Magesha NGWIRI

Kuna jambo linaloudhi kuona jinsi serikali inavyofanya maamuzi muhimu na kuyatangaza kwa watu watakaoathirika zaidi. Labda kuna maelezo yanayoeleweka kuhusu hatua hizo; hakuna serikali inayofurahia kuona ajenda zake zikigeuzwa kuwa mjadala wa kijinga kama inaamini kuwa inachofanya ni sahihi.

Hata hivyo, hatari ni kuwa watu wakibaini kuwa chochote kile, hata kama kinapendwa, kinalazimishwa kwao, wao huonekana kukichukia, na hatimaye kukikataa kabisa.

Utawala bora unahitaji kuwa kila mara washirika washauriwe na maoni mbalimbali yasikizwe, yapimwe kubaini ubora, na ikiwa mabadiliko ya sera yatalenga mazuri kwa wote, hatimaye yatakubaliwa.

Mtindo wa "chukua au uwache" katika uendeshaji wa masuala ya umma sio mzuri katika nchi ya kidemokrasia, kwa sababu hutoa harufu kali ya amri, hata katika hali ambapo kinachosemwa kina manufaa kwa jamii kwa kipindi kirefu. Sauti za wananchi ni muhimu; ushawishi ni muhimu.

### Mtaalamu mwenye uzoefu

Mnamo Jumanne, Wakenya waliamkia habari kwamba shule za msingi za mabweni zitapigwa marufuku kuanzia Junuari mwaka ujao wanafunzi watakaporudi kutoka likizoni.

Katibu wa Idara ya Elimu ya Msingi Belio Kipsang', mtaalamu mwenye uzoefu mkubwa ambaye anaelewa masuala ya elimu kwani amehudumu katika wadhifa huo tangu 2013 - lakini baadaye akahamishwa hadi wizara nyingine mwaka jana kutokana na sababu zisizofaa hapa - hangeibuka na mabadiliko kama hayo makubwa katika sera ya elimu bila kufanya mashauriano.

Kwa hakika, sababu alizotoa kutetea mabadiliko hayo zinaeleweka na yanafaa.

Shida ni kuwa tangazo lake lilishangaza kila mtu, isipokuwa, labda, wenzake katika serikali, uongozi wa Chama cha Kitaifa cha Walimu (KNUT) na walimu wakuu ambao wanaoenekana kuwa na ufahamu.

Kwa hakika, ikizingatiwa kuwa kuundwa kwa sera sio sehemu ya kazi yake, sharti idhaniwe kuwa mkubwa wake, Waziri wa Elimu, alikuwa na ufahamu zaidi.

Kama hali ni hiyo, haileweki ni kwa nini katibu huyo ndiye aliachiwa wajibu wa kutoa tangazo hilo lenye athari za kudumu.

Mtu anaweza kudai kuwa hii ilikuwa mbinu ya kujikinga kutokana na changamoto zilizosababishwa na utekelezaji wa mtaala wa elimu kutoka mfumo wa 8-4-4 hadi ule wa Umilisi na Utendaji (CBC); ambao nchi haijajiandaa kwao.

Dalili ya kwanza kuwa hali itakuwa hivyo ilionekana serikali ilipoamua kuwa Shule ya Upili Tangulizi, inayoanza katika Gredi 7 hadi Gredi 9, itakuwa katika shule za msingi.

Hii ina maana kuwa watoto watakaohitimu kutoka Gredi 6 hawataelekea shule za upili kwa sababu ni shule chache za hadhi hiyo zinaweza kuwahudumia.

Hatua hii ina mantiki. Huwezi kuwapeleka maelfu ya wanafunzi katika shule za upili ambazo tayari zinazongwa na msongamano wa wanafunzi na utarajie shule hizo kuwapa huduma za mabweni.

Na kwa sababu tayari shule za msingi zina vifaa vya kimsingi, kwa nini watoto wasidumishwe mahali ambapo hawatahitaji mabweni, vyumba vya kulia, vitanda, chakula na hata mazahanati?

Mjadala kuhusu iwapo shule za kutwa ni bora kuliko za mabweni umekuwepo kwa muda mrefu. Kumekuwa na muafaka kwamba hivi karibuni, kusomea shule za kutwa kutakuwa bora zaidi.

Ama kwa hakika katika jamii zilizostawi kiuchumi, dhana ya shule ya mabweni imepitwa na wakati, isipokuwa katika shule za matajiri wanakosomea watoto wa watawala. Lakini wakati huu ambapo sera ya usawa imechukua nafasi ya utabaka, mambo kama hayo yanaendelea kuwa historia.

Kwa hakika, jamii kama hizo za matabaka ya matajiri, wanafunzi wanaosomea shule za kutwa hawatarajiwi kutembea kwa miguu hadi shuleni kisha kurudi nyumbani; wanasafirishwa na tawala za mashinani, au na wazazi wao.

Katika hali yetu, hasa katika maeneo ya miji, hilo halitawezekana kwa sababu gharama itakuwa juu zaidi. Hali hii imefanya shule za kutwa kupendelewa zaidi.

Baada ya muda mrefu, shule za mabweni katika kila kiwango zitadidimia na kuisha kutokana na gharama. Mtu hawezi kuelewa ni kwa nini, kwa sababu ni shule chache tu za msingi zinatoa huduma za mabweni.

Ikumbukwe kuwa wengi wetu tulitembea mwendo mrefu kufika shuleni na hiyo haikutuathiri. Leo, haiwezekana kwa mtoto kwenda shule kilomita 20 kutoka nyumbani bila kuonekana kufanya mazoezi ya mbio za Marathon kwa sababu usafiri wa umma unapatikana hata kama haufai kwa watu wa umri mdogo.

### Gharama ya Kisaikolojia

Kuna sababu nzuri kuhusu ni kwa nini kuzima shule za mabweni katika kila kiwango kutaendelea kuvutia wengi, na gharamu ya juu sio sababu pekee. Hakujawa na mantiki katika hali ya wazazi kukwepa majukumu yao na kuyaachia walimu. Mtoto mwenye umri wa miaka saba ni mdogo zaidi kuwa mbali na nyumbani kwa kipindi kirefu, kwani gharama ya kisaikolojia inaweza kuwa isiyopendeza.

Kwa hakika baadhi ya wazazi hupeleka watoto wao katika shule za mabweni kukwepa kutoa utunzaji hitajika, lakini kuna hatari kubwa ya watoto kama hao kukua visivyo na kugeuka kuwa waasi katika miaka ya baadaye.

Kwa maneno Dkt Kipsang' yanayokumbukwa: "Sharti tubuni njia ambayo tunaweza kuwa na watoto wetu na njia ya kipekee ni kupitia masomo ya kutwa…. Hatuwezi kukodisha majukumu yetu kama wazazi, tushirikiane tu na walimu katika malezi."

Bila shaka, kuna nyakati chache ambazo wazazi hawawezi kutunza watoto wao kwa sababu kila mara hutumwa kufanya kazi mbali na nyumbani, lakini hawa ni wachache na hawawezi kutumiwa kujenga sera, na labda njia fulani inaweza kutafutwa kuwashughulikia.

Kwangu, ninaamini kuwa dhana ya shule ya mabweni katika viwango vyote - shule za upili na vyuo - inaendelea kuisha. Na kile ambacho serikali inaweza kufanya ni kuhakikisha mpango wa kuondolewa kwa shule za mabweni una gharama ndogo iwezekanavyo kwa mzazi.

***andrewngwiri@gmail.com***

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*




**Belio Kipsang.** PICHA | MAKTABA

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# habari kwa picha



**Prince Harry na mkewe Megan, wakiwasili kwa sherehe ya Tuzo ya 2022 ya Ripple of Hope katika hoteli ya New York Hilton Midtown Manhattan jijini New York mnamo Desemba 6, 2022.** PICHA I AFP




**Rais William Ruto akutana akutana na James Cleverly, Waziri wa Uingereza wa Mashauri ya Kigeni, Jumuiya ya Madola na Maendeleo na Nairobu Rais Rigathi Gachagua, Mawaziri Kipchumba Murkomen, Alfred Mutua na Moses Kuria na Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja kabla ya sherehe ya kuzindua Mradi wa Reli Jijini Nairobi.** PICHA | PCS



**Mashua ikifyatua fataki mjini Buenaventura, katika Idara yaValle del Cauca, Colombia, mnamo Desemba 7, 2022.** PICHA I AFP



**Picha ya angani ya mlipuko wa volkeno Kaskazini Mashariki mwa eneo la Mauna Loa, Jimbo la Hawaii, Amerika.** PICHA I AFP



**Mzoga wa ndovu wa kike ukiozea ndani ya kidimbwi cha maji baada ya mnyama huyo kulemewa na makali ya kiangazi katika Hifadhi ya Kitaifa ya Wanyama ya Amboseli mnamo Novemba 29.** PICHA I AFP



**Wapigambizi wakishiriki maonyesho ya Krismasi kwa jina 'chini ya maji' eneo la Aqua Planet 63 jijini Seoul, Korea Kusini, mnamo Desemba 8, 2022.** PICHA I AFP



**Mtaalamu katika ofisi ya mwendesha mashtaka akikagua mabaki ya makombora yaliyotumiwa na wanajeshi wa Urusi kushambulia mji wa pili mkuu wa Ukraine wa Kharkivraine mnamo Desemba 7.** PICHA I AFP

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

■ ALIYEKUWA RAIS ANAKABILIWA NA KESI YA UFISADI

# HATUA YA ZUMA NI KUFUATA UPEPO




Aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini Jacob Zuma akiwa mbele ya Tume ya Uchunguzi Kuhusu wa Utekaji wa Serikali inayochunguza madai mbalimbali ya ufisadi katika serikali na mashirika ya serikali jijini Johannesburg, mnamo Julai 19, 2019. PICHA I AFP

## Wachanganuzi wa kisheria wanasema mashtaka ya kibinafsi ya rais huyo wa zamani hayana uhalali wowote mahakamani na hayawezi kufaulu

● Na CHRIS ERASMUS,-MWANDISHI WA NATION, PRETORIA

Ingawa Mahakama ya Kikatiba Afrika Kusini imeamua kuwa rais wa zamani Jacob Zuma hakuwa na sababu za kumuondoa kiongozi wa mashtaka wa serikali Billy Downer kutoka kwa kesi ya ulaghai, ulanguzi wa pesa na ufisadi iliyomkumba Zuma, na kwa muda mrefu, rais huyo wa zamani anaendelea na juhudi za kuanzisha mashtaka ya kibinafsi dhidi ya Downer na mwanahabari mmoja kwa madai ya kosa la ukiukaji wa haki zake za kikatiba.

Maelezo kuhusu masuala haya mawili, yanayotokana na hali ya Zuma kumchukia na kutomwamini Downer, ambayo rais huyo wa zamani anadai anamuonea na hivyo hafai kuendesha kesi dhidi yake, ni sawa na sinema ya uhalifu ya Hollywood.

Downer ndiye aliyemsukuma gerezani, kwa miaka 15, aliyekuwa mshauri wa Zuma kuhusu masuala ya kifedha, kwa makosa hayo 783 yanayotokana na sakata ya uuzaji silaha miaka ya 1990.

Zuma angali anakabiliwa na mashtaka kuhusu sakati hiyo.

Inasemekana kuwa mashtaka ya kibinafsi dhidi ya Downer na mwanahabari wa mahakama, uhalifu na upekuzi, yanatokana na madai ya kuhujumiwa kwa haki ya kikatiba ya Zuma kuhusu usiri wa masuala ya afya yake.

Zuma anadai kuwa Downer "alifuchua" maelezo fulani kuhusu hali yake ya kiafya, kwa mwanahabari Karyn Maughan, na habari hizo zikachapishwa katika chombo cha habari nchini humo Zuma alipokuwa akijitetea kortini kuwa alikuwa mgonjwa kiasi kwamba hangehudhuria binafsi.


Hatimaye hali yake "ya kutokuwa na afya nzuri" ilitajwa kuwa sababu ya kuachiliwa kwake mapema baada ya kuhukumiwa kifungo cha miezi 15 na Mahakama ya Kikatiba mnamo Julai 2021 kwa kudharau maagizo ya mahakama. Sababu hiyo sasa imekataliwa na mahakama.

Mawakili wa Zuma katika kesi hizi mbili na zingine zilizo kortini, walisema rais huyo wa zamani alikuwa "mgonjwa zaidi" na alihitaji kutunzwa kwa saa 24 na hata alikuwa hatari ya kupoteza maisha yake. Lakini hawakubaini

Endelea Uk 12

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Juhudi za Zuma hazitamsaidia




Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini akihutubia wanahabari katika Ikulu ya Nairobi mnamo Novemba 9, 2022. PICHA I FRANCIS NDERITU

Kutoka Uk 11

iwapo hali yake itakuwa mbaya zaidi wakati wowote.

Zuma anatoa maelezo yasiyo kamili katika vyombo vya habari kuhusu alichokuwa akiugua. Lakini anasema Downer alivunja haki yake ya kimsingi kwa kumpa Maughan maelezo aliyodai kuwa ya kweli kuhusu hali yake ya kiafya na kwamba Maughan pia alichapisha maelezo hayo kama mambo ya "kweli".

Lakini wachanganuzi wa masuala ya sheria wanaamini kuwa kesi hiyo haiko kortini kwa njia ya haki na haina nafasi ya kufaulu. Wanasema pia haiwezi kukatiwa rufaa, ingawa mahakama ya chini inaweza kushawishika kuchukua kesi ya Zuma kwa uzito na kuwapata Downer na Maughan na makosa.

Shida kwa Zuma ni kuwa mashtaka yake ya kibinafsi yamekitwa katika masuala mengi ambayo "si sahihi" yanayoweza kuchangia kufeli kwa kesi hiyo katika kiunzi cha kwanza - kutolewa kwa ushahidi wa kweli na utakaokubalika dhidi ya washtakiwa.

Maughan amesema kesi hiyo si kitu bali dhuluma na hatua ya Zuma kukwepa lawama. Amemtaja kiongozi wa mashtaka aliyempa maelezo ya kimatibabu kuhusu Zuma, na mtu huyo si Downer na kwamba alipokea na kuandikisha kuhusu hali hiyo, kwa misingi ya kisheria, baada ya kupata maelezo kutoka kwa stakabadhi za mahakama, na hivyo kutoka kwa rekodi za umma.

Kutokana na hayo, msimamo wa kisheria wa Maughan umekuwa kwamba mashtaka dhidi yake ni ya uongo na ni mkakati mwingine ambao Zuma anataka kutumia kujikinga na hali ngumu mahakamani.

Chini ya Sheria za Afrika Kusini, mashtaka ya kibinafsi yanaruhusiwa viongozi wa mashtaka ya umma wakiamua kutofanya hivyo. Lakini sharti serikali kwanza itoe cheti kuthibitisha kuwa imekataa kushtaki.

Akisisitiza kuwa haki zake zimehujumiwa, Zuma ameitisha cheti kama hicho, baada ya Mamlaka ya Mashtaka ya Umma (NPA) kukataa kuwashtaki "washtakiwa hao wawili", Downer na Maughan kwa madai ya kuvunja haki alizotaja.

Kesi hiyo inaendelea ingawa huenda si kwa muda mrefu, hasa kufuati uamuzi wa Alhamisi wa Mahakama ya Kikatiba, hatua ya mwisho ya Zuma na mawakili wake katika mahakama hiyo.

Hatimaye mahakama hiyo ilifutilia mbali juhudi za kutaka Downer apokonywe wajibu wa kiongozi wa mashtaka katika kesi dhidi yake kuhusu sakata ya ununuzi wa silaha.

Zuma amedai kuonewa na Downer kama sababu yake ya kumkataa. Mawakili wake wameeleza mbele ya korti kadhaa kuwa, Downer kwa "kupendelea", amepoteza wadhifa wake wa "kiongozi wa mashtaka"

Huku Mahakama ya Kikatiba ikitupilia mbali kesi ya Zuma dhidi ya Downer, mhusika mkuu katika jaribio la Zuma kuendesha mashtaka ya kibinafsi, ni hakika sasa kesi ya ufisadi dhidi yake ikirudi Januari 30, 2023, atalazimika kushughulika na Downer kama kiongozi wa mashtaka mkuu katika kesi dhidi yake.


Wachanganuzi wa kisheia pia wanakubaliana kwa kusema kuwa jaribio la kuwafungulia mashtaka Downer na Maughan ni mkakati mwingine ambao Zuma anataka kutumia kujikinga. Mkakati huo umesababisha mashtaka mengi dhidi ya rais huyo wa zamani kuondolewa chini ya viongozi wa mashtaka wanaompendelea.

Lakini Jaji Piet Koen, ambaye hata mawakili wa Zuma wamemsifia kama asiyependelea katika kesi dhidi ya rais huyo wa zamani, mara kadhaa ameelezea kukasirishwa na kucheleweshwa kwa kesi mbele yake, akisema anasubiri uamuzi wa Mahakama ya Kikatiba kuhusu nafasi ya Downer mbele ya korti yake. Koen alisema hatavumilia mbinu zozote za kuchelewesha kesi kutoka kwa Zuma na mawakili wake.

Downer ametaka Zuma alipe gharama kubwa ya kesi iwapo atapoteza katika kesi yake. Aliongeza kuwa vikao vya kusikizwa kwa kesi dhidi yake na mwanahabari Maughan vimepangwa kuanza baadaye 2023. Wakati huo kesi dhidi ya Zuma itakuwa inaendelea ama iwe imekamilishwa. Mashtaka ya kibinafsi ya Zuma dhidi ya Downer na Maughan, hata hivyo, huenda yakakosa kuendelea.

Kuhusu hali ya Zuma kuugua, rais huyo wa zamani alionekana katika televisheni wiki hii alipozuru makao yake ya Nkandla katika mkoa wa KwaZulu-Natal. Alionekana akicheza densi na kundi moja la kanisa huku akipiga miguu chini kwa kishindo ilivyo ada ya kucheza densi katika jamii ya Wazulu. Hakuonyesha dalili zozote za kuudhoofika kimwili ua kuwa mchovu.

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Rais William Ruto (kulia) na Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini wakiwa katika Ikulu ya Nairobi wakati wa ziara rasmi mnamo Novemba 9, 2022. PICHA I FRANCIS NDERITU

Nation Media Group "ePaper Copy"

# kurunzi ya dunia

■ MAISHA YA HOFU YA KUSHAMBULIWA NA KOREA KASKAZINI



Picha hii iliyopigwa Novemba 18, 2022 na kutolewa kutoka kwa shirika la habari la serikali ya Korea Kaskazini la Central News Agency mnamo Novemba 19 inaonyesha kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong-Un (katikati) akikagua zana mpya ya kivita katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Pyongyang. Kim alisema atajibu vitisho vya Amerika kwa silaha za kinuklia, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya serikali. PICHA | AFP

# KISIWA HATARINI YA VITA

## Kutokana mahali kilipo, Kisiwa cha Baekryeong kimekuwa eneo muhimu kijeshi ambalo Korea Kusini imejitolea kulinda kwa vyovyote vile

• AFP

Ni eneo la mbali zaidi la magharibi Korea Kusini, wanajeshi ni wengi kuliko raia, na unaweza kuona Korea Kaskazini kutoka ufuo ulio na ua wa seng'eng'e: karibu katika kisiwa cha Baekryeong, jamii iliyo katika uwanja wa vita.

Kikiwa karibu sana na nchi kavu ya Korea Kaskazini kuliko Kusini, Baekryeong ni ngome: vifaru vinaegeshwa katika pande zote za barabara. Kuna vituo vya walinzi katika kila mlima na fuo za kuvutia zimejaa meno ya zimwi - ngome za simiti zinazofanana na piramidi - kukinga uvamizi.

Korea Kusini ilikabidhiwa usimamizi wa kisiwa hicho cha karibu kilomita 45 mraba mwishoni mwa vita vya Korea miaka ya 1950, lakini wakazi wake 5000 au zaidi kidogo - na idadi kubwa zaidi ya wanajeshi - wanaishi kwa hofu kuu kila wakati.

Kwa miaka mingi kumekuwa na tishio la makabiliano ya kijeshi katika kisiwa hicho: mnamo 2013 Rais wa Korea Kaskazini, Kim alidai anaweza "kunyesha moto" katika Baekryeong, kisha akaanza mazoezi ya uvamizi mwigo mnamo 2017.

"Kuna nyakati huwa ninaota Korea Kaskazini ikivamia, hasa kwa kile kinachotokea katika habari," akasema mzaliwa wa Baekryeong, Kim Keum-sook, mwenye umri wa miaka 64 akimaamisha maonyesho ya makombora makubwa ambayo Kim alizindua mwaka huu.

Kisiwa hicho kina umuhimu mkubwa kwa Korea Kusini, kwa kuwa kinaisaidia kudhibiti njia

Endelea Uk 14

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# Hofu kuhusu makombora ya Korea Kaskazini

Kutoka Uk 13

muhimu za meli kwenye Bahari ya Yellow, ambazo zikikatizwa bandari yake ya Incheon itakatwa kutoka maeneo mengine ya ulimwengu.

Alipokuwa akikua katika Baekryeong, kisiwa kilicho kilomita mbili kutoka mpaka wa baharini na kilomita 14 kutoka nchi kavu ya Korea Kaskazini, Kim alikuwa akihamishwa kila wakati taharuki ilipotanda. "Bado naishi kwa woga," anasema, ingawa mumewe, Choi Won-mo, 65, ambaye pia ni mzaliwa wa kisiwa hicho, alisema "wamelindwa vyema inavyowezekana."

Wanajeshi wa " baharini, angani, majini na nchi kavu wa Korea Kusini wote wako Baekryeong, katika hali ya tahadhari kila wakati," akasema Choi. Mpaka wa baharini umekumbwa na makabiliano ya mara kwa mara, ikiwemo ufyatulianaji wa risasi za kuonyana katika sehemu ya bahari karibu na Baekryeong mwezi Oktoba baada ya meli ya Korea Kaskazini kuvuka hadi eneo Mwisho la Mpaka wa Kaskazini.

Choi alisema matukio kama hayo "ni ya kawaida" lakini baada ya miaka 70 wakiwa katika hali ya kutojua kitakachotokea, watu wamezoea kuishi kwa taharuki - vita vya Korea viliisha kwa makubaliano ya kuvisitisha, na kuacha pande zote mbili zikiwa bado kwenye vita.

Tukio baya zaidi lilitokea Machi 2010, kilomita moja tu kutoka kisiwa hicho, meli ya kivita ya Korea Kusini ilipozamishwa na kile serikali ya nchi hiyo ilitaja kuwa kombora la Korea Kaskazini na kuua mabaharia 46 waliokuwa ndani.

Kwa wakati huu, wanajeshi wa Korea Kusini hufanya mazoezi ya silaha katika ufuo huo. "Hebu tazama hawa wanajeshi wote na silaha hapa, serikali imejitolea kulinda kisiwa cha Baekryeong kwa vyovyote vile," akasema Lee Chung- dong, mvuvi mwenye umri wa miaka 71 ambaye ameishi hapa kwa karibu nusu karne. "Ni kwa sababu wanajua kuwa Baekryeong ikitekwa, pia Incheon itafuatia."


Licha ya hatari zote - feri ya kuelekea kisiwa hicho inapitia njia ya mzunguko ili kuepuka hatari ya kushambuliwa na Korea Kaskazini - Baekryeong ni kituo cha utalii.

Mamia ya watalii hukitembelea kila wiki, kwa kuvutiwa na ukaribu wake na Kaskazini, naumaridadi wake wa kiasili. Kimojawapo cha vivituo vyake ni mwamba unaojulikana kama Dumujin, unaotajwa katika maandishi ya msomi mmoja kwa jina Joseon Dynasty kama "Sanaa ya mwisho ya mungu mzee."

Kivutio kingine ni ufuo wa Sagot na changarawe yake ngumu inayoufanya kuwa uwanja mdogo wa ndege, jukumu ambalo ulitekeleza wakati wa Vita vya Korea. "Umaridadi wa Baekryeong uko katika mandhari yake asili," akasema Kim Yong-sung, 50, aliyekuwa akizuru kisiwa hicho akiwa na wafanyakazi wenzake. "Ninahisi hatari kuwa karibu na mpaka, lakini kwa sababu imekuwa hivyo kila wakati, haitanifanya nisifurahie umaridadi wa hapa."

Mawe ya kale ya kisiwa hicho huwa ni funzo kwa wanaohofia kuwepo kwake kama eneo la vita, anasema Kim Chang-hee, 75, mwelekezi wa mbuga. "Kisiwa hiki kina umri wa zaidi ya miaka 70 - ni cha zamani kuliko viumbe wazee zaidi," akasema. "Korea imekuwa imegawanyika kwa miaka 70. Siku moja, hii pia itakuwa kumbukumbu ya zamani."

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*



Rais William Ruto na Rais wa Korea Kusini Yoon Suk Yeol wakati wa ziara yake ya siku tatu. PICHA | PCS



Rais William Ruto baada ya kufika jijini Seoul mnamo Desemba 9 kwa mazungumzo na serikali ya Korea Kusini. PICHA | PCS

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

WAFANYA KAZI WAMPELEKA ELON MUSK KORTINI

# SHIDA KATIKA TWITTER

## Kesi nyingi zinazomkabili Musk zinaweza kumlazimisha kushauriana na walalamishi kwa sababu kampuni yake iko katika hali mbaya kifedha



Mkurugenzi wa Tesla Elon Musk akizungumza jijini Hawthorne, California, mnamo Machi 14, 2019. Ingawa hatua yake ya kutoa kampuni yaTwitter katika soko la hisa inamruhusu kufanya mabadiliko makuwa kwa haraka, imeingiza kampuni hiyo katika madeni zaidi. AFP

• AFP

Mageuzi aliyofanya bwanyenye Elon Musk katika kampuni ya Twitter mara tu baada ya kuchukua umiliki wake yaliacha nusu ya jumla ya wafanyakazi wake 7,500 bila ajira.

Kwa sasa, wengi wao wameamua kumshtaki mahakamani mmiliki huyo wa kampuni za SpaceX na Tesla.

Mtandao huo wa kijamii unakabiliwa na kesi nyingi kutokana na jinsi watu hao walivyofutwa kazi - hata malalamishi kwa jiji la San Francisco kuwa Musk amebadilisha eneo la ofisi kuwa vyumba vya malazi kuwezesha wafanyakazi kulala wakiwa bado kazini. "Ni inasikitisga kuwa mtu tajiri zaidi duniani anafikiri anaweza kukiuka haki za wafanyakazi wote bila kufuata sheria. Tunalenga kuhakikisha kuwa anawajibika," akasema wakili Shannon Liss-Riordan.

Liss-Riordan anaongoza kesi kama hiyo dhidi ya Twitter – inayosema kuwa baadhi ya wafanyakazi hawapati malipo na fidia waliyoahidiwa kabla ya Musk kuchukua usukani.

Ahadi hizo, ambazo zilijumuisha bonasi, zilitolewa kushawishi wafanyakazi hao kubakia katika Twitter. Waliahidiwa malipo mazuri ya kuondoka baada ya Musk kuanza kuhudumu kama kiongozi na mmiliki wa kampuni hiyo.

Kesi nyingine zinahusu hatua ya Musk ya kutoa makataa kwa wafanyakazi wake kutia saini makubaliano kuhusu ruwaza yake ya kampuni hiyo na kukumbatia "mtindo mkali" wa kufanya kazi, au kuchukua mshahara wa miezi mitatu na kuondoka.

Hilo, mawakili wanasema, ni mpango wa makusudi kuwafuta kazi unaokiuka sheria ya jimbo la California, kuwanyima wafanyakazi malipo yao na kuwapa notisi kwa muda wa siku 60 inavyotakiwa kisheria.

Hatua ya Musk ya kupinga mfumo wa watu kufanyia kazi nyumbani kwao pia unapingwa, kwani anawaagiza wafanyakazi walemavu au wanaougua wafika ofisini kufanya kazi na inaonekana kuwa ubaguzi.

"Kuna ukiukaji mkubwa wa masuala ya kibinafsi, kama vile watu wenye matatizo maalumu ya kiafya. Haya yote yalifanywa Elon Musk alipokuwa akitutukana hadharani katika Twitter," akasema Amir Shevat, aliyekuwa mfanyakazi wa cheo cha juu katika kampuni hiyo.

Shevat na wafanyakazi wengine wanawakilishwa na Lisa Bloom, wakili maarufu jijini Los Angeles, ambaye amemwakilisha produsa wa sinema za Hollywood, Harvey Weinstein.

Bloom anasimamia mchakato wa maelewano baina ya kampuni hiyo na wafanyakazi wake, kwani wafanyakazi wengi walitia saini mpango wa kuwazuia kutetea haki zao mahakamani walipojiunga nayo. "Tutaendelea kuwasilisha kesi hizi, moja baada ya nyingine," akasema Bloom kwenye kikao na wanahabari Jumatatu. "Tuko tayari kushughulikia kesi hizi bila kujali wingi wake ili kuhakikisha wafanyakazi hao wamelipwa malipo yao," akasema.

Wataalamu wanasema huenda hilo likamgharimu Musk pakubwa. "Huenda Twitter ikaamua kusuluhisha suala hilo haraka kwa kuwalipa wafanyakazi wake wa zamani malipo wanayoidai kulingana na sheria," akasema Eric Goldman, ambaye ni profesa wa sheria katika Chuo Kikuu cha Santa Clara.

"Au huenda ikakataa kulegeza msimamo wake, hivyo kuwafanya kuhangaika, hali ambayo huenda ikachukua miaka mingi," akasema.

Idadi kubwa ya kesi hizo huenda ikamfanya Musk kuamua kufuata njia ya maelewano nje ya mahakama, ikizingatiwa kuwa kampuni hiyo inakabiliwa na changamoto za kifedha baada ya Musk kulipa Sh5.1 trilioni kuimiliki.


Bwanyenye huyo hajazungumzia lolote kuhusu kesi hizo, akionekana kuepuka ukosoaji baada ya vyumba vya mikutano vya Twitter kugeuzwa kuwa vya malazi.

"Kwa hivyo jiji la San Francisco huwa linashambulia kampuni kwa kuweka vitanda kwa wafanyakazi waliochoka badala ya kuhakikisha watoto wako salama dhidi ya matumizi yasiyofaa ya dawa ya fentanyl," akasema Musk kwenye ujumbe alioweka katika Twitter, akimshambulia Meya London Breed.

Musk alikuwa akizungumzia tukio la juzi, ambapo mtoto wa miezi kumi alikunywa dawa hiyo kupita kiasi katika uwanja mmoja wa michezo.

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media


SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM